Kumwita Yesu Jukwaani

Tunasoma Neno la Bwana. Katika Injili ya Mathayo, m—mlango wa 8, kuanzia kifungu cha 23, tunasoma hivi.

Akapanda chomboni, wanafunzi wake wakamfuata.

. . .kukawa na msukosuko baharini, hata chombo kikafunikizwa na mawimbi, naye alikuwa amelala usingizi.

Wanafunzi wake wakamwendea, wakamwamsha, wakisema, Bwana, tuokoe, tunaangamia.

Akawaambia, Mbona mmekuwa waoga, enyi wa imani haba? Mara akaondoka akazikemea pepo na bahari; kukawa shwari kuu.

Wale watu *wakamaka wakisema, Huyu ni mtu wa namna gani hata pepo na* bahari *zamtii?*

2 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa maombi.

3 Baba yetu wa Mbinguni, tuna furaha sana usiku wa leo kujua ya kwamba Mtu huyu mkuu ambaye hufanya pepo na bahari kumtii yu pamoja nasi. Tuna shukrani kwamba tuna ushuhuda huu mkuu wa uhai Wake hata leo, na tukijua kwamba Yeye ni wa Milele, wala hawezi kufa. Yu hai milele, na ametuonyesha rehema Zake kuu, sisi wanadamu katika siku hizi. Sisi ni wahitaji, Bwana, wahitaji sana hivi kwamba hakuna mwingine anayeweza kutimiza mahitaji yetu ila Wewe. Kwa hiyo tunakutazamia Wewe usiku wa leo kuja kwenye mkutano wetu hapa, na kujitambulisha Mwenyewe kwetu, kwa kusamehe dhambi zetu, kuongeza imani yetu, Bwana, na kuponya magonjwa yetu na mateso. Na wakati tukienda nyumbani mwetu, usiku wa leo, jalia tuwe na furaha, tukisema kama wale waliotoka Emau, “Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo aliposema nasi njiani?” Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

Mwaweza kuketi.

4 Mimi karibu ni kama Zakayo; mambo haya daima huwa mafupi sana kwangu. Ninataka kuwazungumzia kwa muda mfupi tu sasa kabla hatujawaombea wagonjwa. Nikiwashukuru kwa ushirikiano wenu mwema, na kuamini katika Roho, jana usiku, tulipokuwa tukizungumza, tukitumaini kwamba utakuwa ni umwagikaji mkuu wa baraka Zake.

5 Daima kumbukeni kile kilichotuleta hapa, ni kujaribu kuzidisha imani yenu katika Uwepo Wake, ili mweze kupokea kile mnachoomba. Halafu, kwa imani, mnaamini.

6 Sasa, kumbukeni, kila baraka ya ukombozi imenunuliwa tayari. Gharama imelipwa, ipo njia noja tu ambayo kwayo utaweza kuipokea, ni kuiamini na kuikubali. "Yeye ni Kuhani Mkuu wa maungamo yetu." Waebrania inasema hapo, waraka wa Waebrania, unasema, "Yeye ndiye Kuhani Mkuu wa maungamo yetu." Kuungama, na kukiri, ni kitu kile kile, bila shaka. Kwa hiyo sisi . . . Yeye ndiye Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, kwa hiyo hawezi kututendea chochote mpaka kwanza tuungame kwamba amekitenda. Ndipo basi tunapokiungama, basi Yeye ni Kuhani Mkuu, mwombezi, kuingia kazini juu ya hicho na kukiweka sawa. Kwa hiyo tunaomba, tukimtumainia Mungu usiku wa leo, katika fadhili Zake na rehema, kwamba atatupa wingi wa neema Yake, usiku wa leo. Na sasa, kumbukeni, huna budi kuikubali.

7 Sasa tunaenda kuombea wagonjwa kabla hatujaondoka, tukiwawekea mikono, lakini natamani mngalikuwa na imani ya kutosha isiwabidi kuwekewa mikono. Laiti mngaliinuka tu na kusema, "Bwana Yesu, ninakuamini. Mimi—mimi . . . " Yeye analiamini Neno.

8 Sasa, mnaona, Mungu ni tofauti na jinsi tulivyo. Ikiwa—ikiwa tungekuambia ufanye jambo fulani, nawe usiliamini, vema, tungesema, "Achana nao. Si lazima waliamini." Lakini huyo si Mungu Baba yetu. Yeye daima atafanya jambo lingine kukufanya uamini. Anajaribu kudumisha Neno Lake, na Yeye atalitimiza Neno Lake.

9 Sasa sababu ya Yeye kufanya mambo anayofanya sasa, ni kwa sababu aliahidi kuyafanya. Si kwamba inamlazimu kuyafanya; bali aliahidi kuyafanya, na hiyo ndiyo imani yetu kwamba Yeye daima hutimiza ahadi Yake.

10 Sasa kila mmoja wenu, ukiwa na wapendwa wako, wagonjwa, na kadhalika, wameketi, ikiwa hawawezi . . . kama huyu msichana mdogo hapa, yeye ni mdogo sana, naye yuko katika hali hiyo alimo; wakati tu ukiamini, weka mikono yako juu ya mtoto huyo huku ibada ikiendelea. Wengine, mlio na wapendwa wenu, moyoni mwenu mnawaza kuwahusu; kwa imani wainueni moja kwa moja mbele za Mungu, katika maombi. Sasa, na, kwa hiyo, amini basi. Jambo fulani likitendeka, wewe . . .

11 Huwezi kujifanya mwenyewe kuamini. Wewe, ni kitu fulani, ni sifa iliyo ndani yako. "Imani ni kuwa na hakika," si tu dhana za kujibunia. "Ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, bayana ya mambo unayoamini, wala huyaoni." Na yote, silaha zote za Ukristo sasa, kumbukeni, ni kwa imani. Yote ya kimbinguni, upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, upole, subira, hayo yote ni mambo yasiyoonekana. Hizo ndizo silaha zote za Ukristo. Mkristo daima huangalia mambo ambayo hayaoni, kwa sababu anaangalia ahadi.

12 Hapa wakati fulani uliopita, miaka mingi, niliitwa mahali, wakati mmoja, katika hospitali, kumwombea mvulana aliyekuwa akifa, kwa dondakoo. Nimetaja hili mara nyingi, maana ni kisa kisichosahaulika kwangu mimi. Baba yake alikuwa mzee, na mama. Naye kijana huyu alikuwa na yapata umri wa miaka kumi na minne, nadhani, naye alikuwa mtoto wao wa pekee. Naye alikuwa akifa, kwa dondakoo, na jambo fulani likafanyikia moyo wake. Alipoteza fahamu. Nao walikuwa tu . . . Yeye aninii, loo, a—alikuwa hai kwa shida sana; nasahau kile ma—mapigo ya moyo wake ulichokuwa; kupumua kwake kulikuwa chini sana.

13 Naye maskini baba yake alishikilia kuja kwenye mkutano, na kusihi, kumwona meneja, na kila mtu. "Njoo, uombe! Njoo, uombe! Hayo tu, njoo tu hospitalini ukaombe."

Meneja akasema, "Mlete kwenye mkutano."

14 Kasema, "Hatuwezi kumtoa hospitalini. Yuafa." Pia kasema, "Kama Ndugu Branham angekuja tu, amwombe Mungu, Mungu atalijalia."

Nikawaza, "Imani ya jinsi gani!"

15 Nikaenda hospitalini, nao madaktari wasingeniruhusu kuingia. Wakasema, "Hapana, wewe ni mtu uliyeoa, una watoto." Billy Paul alikuwa mdogo wakati huo. Kasema, "Huwezi kuingia," kasema, "kwa maana una mtoto."

16 Nami nikasema, "Sasa, nimesikia ya kwamba daktari mwenyewe alikuwa ni Mkatoliki." Nikasema, "Kama kasisi alitaka kumfanyia mtoto huyo kaida za mwisho, kama yeye ni Mkatoliki, ungemruhusu aingie?"

17 Kasema, "Hiyo ni tofauti. Kasisi hana watoto." Unaona? Kasema, "Wewe waweza kubeba mdudu huyo na kumpelekea mtoto wako."

18 Ndipo nikasema, "Lakini, angalia, bwana. Acha nichukue jukumu. Nitatia sahihi karatasi. Nitachukua jukumu. Kama sina imani ya kutosha kuingia mle kwa sababu ya hiyo, basi sina shughuli ya kuingia humo, kwanza kabisa." Nikasema basi, "Lakini nitachukua jukumu." Tena nikasema, "Liwazie sasa, kama huyo mvulana angekuwa ni Mkatoliki, naye alikuwa yuafa; basi je! ungeweza, kwa njia yoyote, kumzuia kasisi asimpe kaida za mwisho za kanisa?"

Akasema, "La, nisingefanya hivyo."

19 Nikasema, "Mimi kwao ni kama tu kasisi alivyo kwa Wakatoliki."

20 Ndipo akasema, "Sawa," na hatimaye akakubali. Akanivalisha kama Ku Klux Klan, wa namna fulani, vitu hivi vyote juu yangu, na—na kunipeleka mle kwa mvulana huyu mdogo, akifa.

21 Mama na baba wakapiga magoti upande ule mwingine. Ndipo nikaomba tu maombi mafupi rahisi, "Bwana Yesu, ninakutumainia kumwinua mvulana huyu, kwa ima- . . . msingi wa imani ya huyu baba na mama," nikaweka mikono yangu juu ya jamaa huyu mdogo. Alikuwa amepoteza fahamu kwa ninii tatu, yapata siku tatu, naamini, huku akipumua kwa shida. Ndipo nikasimama, nikasema, "Amina." Nikaomba kama dakika moja, kisha nikasimama.

22 Ndipo huyo baba mkongwe akamshika mama kwa mikono yake, na akasema, "Liwazie, mpenzi, mvulana wetu amepona!" Hakuna dalili yake hata kidogo. Nao walikuwa wanakumbatiana tu, na kumshukuru Bwana.

23 Naye maskini nesi, mtoto mdogo, msichana, hasa, alikuwa labda na umri wa yapata miaka kumi na minane, ishirini. Alikuwa na utepe wake wa nesi, naye . . . ama, alikuwa nesi aliyehitimu. Ndipo akasema, "Bwana, ninahofia huelewi." Akasema, "Mvulana huyu anakufa."

Akasema, "Loo, hapana. Mvulana huyu ataishi." Baba akasema.

24 Pia kasema, "Unawezaje kujiadhibisha hivyo na nanii wako . . . unajua mvulana wako yuafa, chini ya mawazo ya uongo kama ulivyopewa?"

Kasema, "Hayo siyo mawazo mapotovu." Yeye . . .

25 Akasema, "Tazama." Sasa huenda nikaninii . . . Huenda kuna daktari aliyepo ameketi hapa sasa. Sijui haya kuhusu tiba, na vifaa vya istilahi za tiba. Walimfanyia namna fulani ya kadiogramu, na moyo wake ulikuwa chini sana. Ulikuwa umekuwa chini muda huo wote. Daktari akasema . . . Nesi akamnukuu daktari, kasema yeye . . . "Hiyo haijawahi kuonekana kote katika historia, moyo ukienda chini namna hiyo, kuwahi kuamka tena."

26 Kamwe sitasahau mtazamo wa huyo mzee. Jamaa mkongwe aliye na ubaba alitembea na kuweka mkono wake kwenye bega la maskini nesi huyo. Akasema, "Sista," akasema, "unaona, unaangalia kwenye ile chati." Kasema, "Hayo ndiyo yote ujuayo, ni kutazama hiyo. Ila," kasema, "mimi ninaangalia ahadi ya Kiungu."

27 Huyo mvulana ni mmishenari kule Afrika sasa, anao watoto watatu. Mnaona? Mnaona? Inategemea kile unachoangalia, unaona. Aliamini.

28 Sasa, hiyo ni imani ile ile, "Kama utakuja uweke mikono Yako juu ya mtoto wangu. Kama utanena neno, mtumishi wangu . . . " Unaona, hicho ni kitu fulani ulicho nacho. Wewe—wewe . . .

29 Basi halikuwa—halikuwa ni tendo la kujifanya. Mzee huyo aliamini hilo. Alikuwa ameshikilia Kitu fulani.

30 Yule mwanamke aliyegusa vazi Lake. "Kama itanibidi tu kuligusa vazi Lake!" Jambo ndilo hilo. Huna budi kuishikilia imani hiyo, ndani ya moyo wako. Ni kama tu vile unasema . . .

31 Unajua, ewe mwanamume, ikiwa wewe ni—ikiwa wewe ni aina ya mume anayefaa, hakuna mwanamke duniani unayempenda kama mke wako. Huenda kuna wanawake wengine ambao huenda ni warembo zaidi. Huenda kuna wanawake ambao—ambao ni wanawake wa—wa—warembo zaidi, na kadhalika. Bali kitu fulani, kama kweli unampenda mke wako, kuna kitu mle ndani ambacho huoni sura yake. Unampenda. Na wewe—wewe hujui ni kwa nini, bali unampenda. Na, wanawake, vivyo hivyo wewe kwa mume wako. Wewe, unampenda. Nanyi wasichana wadogo kwa wapenzi wenu wavulana; wapenzi wavulana kwa mpenzi msichana. Kama umekutana na mtu huyo unayejua unampenda, kuna kitu humo ndani unajua unampenda.

32 Vema, ni vivyo hivyo kuhusu imani. Unajua litatendeka. Hakuna shaka, haijalishi ni wangapi wangesema kinyume; ungali unaamini jambo lile lile, kwa sababu hiyo ni ya kweli, imani halisi ya kweli. Sasa uwe na hiyo usiku wa leo, wakati tukizungumza juu ya somo hili.

33 Nilizungumza sana, na nimekuwa kwenye mikutano muda mrefu sana sasa, sijapata kupumzika, hata kidogo, tangu Krismasi. Nami kidogo nimepwelewa na sauti kooni mwangu, kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, na wakati, na kadhalika.

34 Ninataka kuwazungumzia usiku wa leo juu ya somo la, "mwamshe Yesu," ama: *Kumwita Yesu Jukwaani*.

35 Kutokana na somo letu la Maandiko, tunaona ya kwamba kulikuwa na mkutano mkubwa. Yesu alikuwa akizunguka, akifanya miujiza mikuu, kila mara akitenda mema, na pia akitenda yale yaliyompendeza Mungu. Daima alimpendeza Mungu, bali hakujipendeza Mwenyewe, Biblia ilisema. Nasi tunaona kwamba Mwenyewe alijitambulisha kabisa, kwamba alikuwa ni Nani, kwa kazi Zake. Kazi Zake zilimtambulisha kuwa ni Nani.

36 Na nguvu zilikuwa zimemtoka. Alikuwa akifunza mafumbo, siku nzima, na nguvu zilikuwa zimemtoka. Naye alikuwa . . . alikuwa anaenda kuvuka bahari, kwenda ng'ambo, upande ule mwingine. Kwa kuwa kile alichokuwa, Yeye—Yeye alijua kulikuwa na kazi kubwa mbele, upande ule mwingine. Naye alikuwa amechoka sana. Nguvu zilikuwa zimemtoka, siku nzima, kwa kuwa watu walikuwa wamemgusa kwa imani yao, kumwamini, na kadhalika. Naye alikuwa . . .

37 Nguvu zilikuwa zimemtoka, Naye alikuwa amechoka. Kwa hiyo akaenda nyuma ya merikebu na akalala chini kwenye mto, Maandiko yanatuambia, kupumzika kidogo wakati merikebu

ikivuka bahari, ikivuka Bahari ya Galilaya, fursa ya kupumzika kidogo.

38 Wanafunzi Wake wakachukua makasia yao, na kuinua matanga, na kama tu mabaharia wangefanya. Hao, hiyo ndiyo ninii yao, wengi wao, kazi yao. Walikuwa ni wavuvi hapo baharini, na—na walijua jinsi ya kuendesha hizi merikebu. Nao walikuwa wamerejea kwenye kazi yao, wakiwa tu na wakati mzuri wa kufurahia, wakati wa furaha, labda wakizungumza juu ya mambo yaliyotukia siku hiyo.

39 Mnajua, kuna kitu kuhusu hilo, kwamba wakati tukimwona Bwana wetu Yesu akifanya mambo, na tunaweza kujua kwamba ni Yeye, kwamba hakuna chochote kingine kingaliweza kufanya hayo ila Yeye, sisi kwa urahisi. . . Tukikutana pamoja, sisi . . . Kila mtu anataka kushuhudia. Kila mtu anataka kusema jambo fulani, na wanataka kuzungumza juu yake. Mnaweza kuwa na uamsho kanisani mwenu; mchungaji anaweza kuhubiri ujumbe wa ajabu, ama mwinjilisti, ama yeyote yule; ama mnaweza kuona jambo fulani likitendeka, ama kitu fulani katika ujirani, mtu fulani aliponywa. Majirani wanajumuika pamoja na kuzungumza juu ya hilo. "Jinsi lilivyo la ajabu! Ulikuwapo? Ungepaswa kuliona. Lilikuwa ndilo jambo la ajabu kuliko yote." Kuna kitu kuhusu kazi za Mungu ambacho husisimua moyo wa mwanadamu kuliko chochote kingine kinachotendeka. Kuna . . . Ni matukio yasiyosahaulika kabisa tunapokutana na Bwana Yesu na kuona mambo anayotenda, ni kuu sana na za ajabu njia Zake.

40 Sasa tunaona ya kwamba walikuwa wakifurahia kazi zilizokuwa zimefanywa katika uamsho wa siku hiyo, na labda ningefananisha sisi, usiku wa leo, kuwa vivyo hivyo.

41 Sasa ndiyo kwanza tushuhudie moja ya miamsho mikuu kuliko yote, ninaamini, ulimwengu uliowahi kushuhudia, katika miaka hii kumi, kumi na tano iliyopita. Umekuwa ni u—uamsho, sio tu kama siku za Billy Sunday, ama siku za uamsho wa Welshi, ama siku za—za uamsho wa Wesley, ama uamsho wa Moody, ama uamsho wa Billy Sunday. Umekuwa ni kitu kinachoenea duniani kote, kote ulimwenguni. Ibada kuu za uponyaji na mioto mikuu ya uamsho kwa kweli imewaka juu ya kila kilima kilichoko duniani. Moja kwa moja usiku wa leo, mbali kule katika nchi za Afrika, huko chini Uchina na Japan, Injili hii inahubiriwa, na watu wanaponywa dakika ii hii, kote na kote ulimwenguni. Umekuwa ni moja ya miamsho mikuu kuliko yote, kwa kuwa, ninaamini, ni moja ya miamsho ya mwisho itakayotukia katika ulimwengu huu, uamsho unaoenea kote ulimwenguni.

42 Lakini sasa, katika miaka michache iliyopita, umepoa. Huoni msisimko ndani ya watu, uliokuwepo hapo nyuma.

43 Ninakumbuka kuwa na majaliwa, kwa Roho Mtakatifu, kuongoza uamsho huo ulioanza, wakati yule Malaika wa

Bwana alipoonekana pale mtoni na kusema hilo, yapata miaka mingi iliyopita. Na kuliona likitendeka, na kuliona likiiwasha mioto mioyo ya wahudumu, kila mahali, miamsho ikaanza. Mbona, ungeweza tu kuingia kwa urahisi kwenye jengo, na watu wanaamka tu kutoka kwenye vijitanda vyao vya wagonjwa na machela, na kuondoka wakitembea, wamepona. Hata haikukubidi kusema neno moja. Ku—kuwepo tu pale, hayo ndiyo tu yaliyohitajika.

44 Ninakumbuka usiku mmoja huko Vandalia, Illinois. Niliingia mkutanoni, na sikuwa nimekaa mkutanoni dakika tano, na hapakuwapo na mtu yeyote dhaifu hapo, mahali popote. Viti vya magurudumu vilitolewa na kulundikwa. Vipofu walikuwa wanaona, na viziwi na bubu wakizungumza, na—na kwa urahisi tu ili . . . Roho wa Bwana alikuwepo, na Yeye aliliponya tu kundi lote la hao. Sasa hapo ndipo unapoweza kufanya jambo, wakati uamsho ukiendelea. Lakini hebu huo moto wa uamsho uzimie, basi ni vigumu kwako . . . Watu wangali ni Wakristo, bali hawahuishwi kuingia kwa Roho huyo, yale mazingira makuu ambayo hufanya jambo.

45 Ni kama tu katika meko ya kufulia chuma, kwenye karakana ya mhunzi. Inakubidi kukifanya chuma kuwa moto kabla ya kuanza kukitwanga kwenye fuawe. Usipofanya hivyo, kamwe hutakinyoosha.

46 Na hiyo ndiyo inayohitajika kuwa na uamsho, ni kila mtu chini ya joto la Roho Mtakatifu ambalo limeshusha nguvu za Mungu na uamsho ukiendelea. Ndipo kuna mikutano ya maombi ikiendelea, mchana na usiku, kila dakika, kila mahali. Mbona, watu hata hawataweza kuondoka hapo!

47 Ninakumbuka huko Jonesboro, Arkansas, wakati nilipoanza ninii yangu kwa mara ya kwanza . . . yapata mkutano wangu wa tatu. Kwanza huko St. Louis, halafu huko Corning, na kisha huko chini Jonesboro. Gazeti lilisema, "Watu elfu ishirini na nane kwenye mkutano." Maili ishirini ama thelathini kutoka mjini, yalikuwa ni mahema tu yamewekwa. Usingeweza kupata nyumba ya shambani kukalia, mji mdogo wa Jonesboro. Na watu wakitoka maili nyingi, wamebeba kandili, wakitembea kupitia misituni, wapande ba—basi na kuja.

48 Niliketi nje nyikani jioni moja, nikiomba kabla ibada kuanza, ndipo nikaona wasichana wakija wamebeba viatu vyao na stokingi chini ya makwapa yao. Ndipo kabla hawajafika kule chini, wanasimama na kupangusa mavumbi kutoka kwenye miguu yao, na kuvaa stokingi zao na—na—na viatu, na—na kuingia mkutanoni.

49 Tena nikawaona wakiwalaza watoto wao wagonjwa chini ya malori ya pamba yaliyochakaa, na kubakia hapo mchana na usiku; wakiwafunika kwa karatasi na magunia, huku

kukinyesha, dhoruba zikivuma; wasiondoke mahali pao, wakingojea tu kuingia ndani ya jengo.

50 Hapo ndipo vipofu walikuwa wanaona, viziwi wanasikia. Nayo huduma, usiku wa leo, iko maili mia moja zaidi ya hapo, ila mioto ya uamsho imefifia.

51 Unaona watu wakitembea pale na kusema. . .Nyosha tu kidole chako, na useme, "Vema, unaamini, ndugu?" Hayo tu, alikuwa amechoka kabisa. Hayo ndiyo yote yaliyobidi kufanywa. Waliamini. Uamsho ulikuwa unaendelea.

52 Sasa, wanafunzi hawa walikuwa wameona hayo, na kwa njia ndogo walikuwa wakiishi hiyo furaha, huku Yesu akipumzika, kwa yale waliyokuwa wameona yakitendwa siku hiyo.

53 Nami nafikiri uamsho unafanya jambo kama hilo, kwamba sasa tunaishi tu katika wakati wa utulivu, huku akipumzika labda kati ya mikutano, ama uamsho na Kuja Kwake. Nasi tunafurahia mambo ambayo tumeona yakifanywa kwenye wakati wa uamsho huu, matendo makuu na ya ajabu. Haijalishi ulimwengu unasema nini, bado tumeliona likifanywa! Ni tamko, ni ukweli wa mambo, lilitendeka.

54 Hapana budi waliichukua fursa, wakati safari ilikuwa shwari, kuzungumza juu Yake, juu ya matendo Yake, juu ya madai Yake, juu ya Umasihi Wake. Wengi wao huenda. . . wa hawa wanafunzi, huenda walinena juu ya yale waliyoona yakifanywa, mmoja kwa mwingine.

55 Kama tu tufanyavyo sisi, wakati wa uamsho huko Shreveport, wakati wa uamsho kwenye—kwenye mji mwingine, tutaongea juu yake.

56 Sasa hivyo ndivyo walivyokuwa wakifanya. Labda ilikuwa ni Simoni, kama tulivyozungumzia jana usiku, akisema, "Vema, wakati Andrea aliponiambia kumhusu, kidogo nilikuwa ninashuku. Lakini wakati Yeye aliponiambia kuwa mimi ni nani na kuwa baba yangu ni nani, hiyo iliniondolea mashaka yote. Ni—niliamini hapo."

57 Huenda ilikuwa kwamba Filipo labda alisema, baadhi ya lile lingine; huenda alikuwa ni Andrea alisema. Tulizungumza kuhusu yule mwanamke kisimani, jana usiku. Huenda walikuwa wakizungumza juu yake, waliposema jambo kama hili, "Ndugu, mnajua, wakati wangu wa ajabu ulipokuwa, wakati mimi—tuliondoka kwenda kununua chakula. Ndipo tukarudi na tulikuwa tumesimama nje ya vichaka, na kumwona akizungumza na mwanamke huyu mwenye sifa mbaya. Tuliwaza, mioyoni mwetu, 'Vipi kama baadhi ya makuhani wangekuja na kuona haya, Bwana wetu akizungumza na mwanamke wa jinsi hii, wangesema nini kumhusu?' Ndipo basi tunakumbuka jinsi tulivyojua, tuliokuwa na imani Naye, kwamba ilikuwa ni kwa kusudi fulani alikuwa akizungumza naye.

58 "Ndipo basi alipomwambia, 'Nenda kamwite mumeo mje naye hapa.' Naye mwanamke akasema, 'Sina mume.' Jinsi mioyo yetu ilishushwa, maana tulidhani huo hapo ni wakati mmoja kuna kushindwa. Yesu alikuwa amemwambia mwanamke huyo kwamba ilimbidi, amwite 'mume' wake, wakati hana mume. Unakumbuka vile tulivyoangaliana uso mmoja na mwenzake huku tukistaajabu, kuwazia ya kwamba imani yote tuliyokuwa nayo Kwake, na hapa ilikuwa imeshushwa ghafula?

59 "Halafu tunaona, mara Yeye akanena na kusema, 'Umesema kweli, kwa kuwa umekuwa na waume watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.'

60 "Ndipo wakati alipomtambua Yeye basi kuwa Masihi, Masihi wa Mungu, na kusema hapo, kwamba, 'Tunajua kwamba Masihi yuaja. Hapana shaka wewe ni Nabii, kwa kuwa tunajua, ajapo Masihi, Yeye atafanya jambo hili.' Nao ushuhuda katika mji huo, ushuhuda wa mwanamke huyo ulikuwa na athari juu ya maisha ya watu wa mji huo."

61 Halafu huenda ilikuwa ni kijana Yohana aliyesema, "Mnajua, nitawaambieni kilicholifanya halisi kwangu, siku ile alipoumega mkate. Sasa, sote tulikuwa na njaa, na Yeye alikuwa ameenda huko nyikani, nasi tusingeweza kumpata, na hapo tukakutana Naye. Basi umati wote ukaja karibu, na, muda si muda wajua, tukamkuta akisema, 'Watume huko mjini, wakanunue chakula.' Ndipo—ndipo akatwambia 'tuwape chakula' basi. Naye akachukua zile biskuti tano na samaki wawili wadogo, kisha akaumega mkate. Nami nikaona mkono Wake wakati angeunyosha tena kuchukua kipande kingine cha mkate, biskuti hiyo iliongezeka tena. Na ndipo alipounyosha tena, akauweka kwenye sahani, kisha akanyosha tena, samaki huyo alikuwa ameongezeka tena. Si tu samaki wa kawaida, bali alikuwa ni samaki aliyepikwa, unaona, tayari ameongezeka tena.

62 "Ni atomu ya aina gani aliyoifungulia, ndugu, samaki aliyepikwa, mkate uliopikwa, acha kukua? Nasi tulijua Yeye alikuwa ni Muumba, lakini hapa Yeye anaumba samaki waliopikwa tayari na mkate uliopikwa."

63 Yohana huenda alisema jambo kama hili. Akasema, "Mnajua, nilipokuwa mvulana mdogo, tuliishi huko karibu na Yeriko. Ninamkumbuka mama yangu wa Kiyahudi alikuwa akinibembeleza nilale wakati wa alasiri; nipate usingizi wangu kidogo wa alasiri. Nilikuwa nikimtazama usoni mwake, naye angenisimula hadithi za Biblia."

64 Na, mnajua, hilo ni jambo jema kwa mama yeyote kumfanyia mtoto wake. "Mlee mtoto katika njia impasayo." Ingekuwa bora kuliko kufungua televisheni na kutazama baadhi ya mambo haya hapa ambayo huendelea kwenye televisheni.

Ungekuwa bora zaidi kama ungemsomea hadithi ya Biblia, maana inajiandika katika moyo wake mchanga.

65 Sasa akasema, “Alizoea . . . Alizoea kuniambia kuhusu ha—hadithi ya yule mwanamke Mshunami akifufuliwa mvulana wake mdogo, na nabii Eliya. Niliipenda hiyo. Tena alizoea kuniambia kuhusu watu wetu kutoka Misri. Nasi tulikuwa moja kwa moja kwenye mto Yordani. Naye angeelekeza ng’ambo ya mto, na kusema, ‘Yohana, walipiga kambi upande ule mwingine. Nao walikuwa miaka arobaini kwenye hilo nyika, na Mungu akawalisha mana. Nguo zao hazikuchakaa. Naye Mungu aliwapa mkate, mpya, kila asubuhi.’

66 “Na jinsi maskini, moyo wangu wa kitoto, nilikuwa nikisema, ‘Mama, je! Mungu anayo matanuri mengi makubwa huko juu angani, Naye huoka mikate hii yote, na huwaweka Malaika Wake tayari kuleta mkate wa asubuhi na kuuweka kwenye . . .?’

67 “‘La,’ angesema. ‘Yohana, wewe ni mdogo sana huwezi kuelewa. Unaona, Mungu hana matanuri angani. Hahitaji matanuri. Sisi lazima tuwe na matanuri. Bali Mungu hayahitaji, maana Yeye ni Muumba. Unaona, Yeye hunena tu, na mkate unakuwa kwenye . . . Yeye ni Muumba.’

68 “Basi, ndugu, niliposimama hapo leo na kumwangalia akichukua kipande hicho cha mkate na kumega huo, na aliponyosha mkono kuchukua kipande kingine, kiliumbwa, nilifahamu hatukuwa tukifuata—tukifuata nabii wa uongo. Huyo alikuwa ni Muumba, Mwenyewe, ndani ya Mwanadamu.” Na ninii . . .

69 Ndipo huenda walizungumzia misimamo ya baadhi ya watu; baadhi waliamini, wengine hawakuamini; na kisha mtazamo Wake juu ya watu.

70 Sasa, unajua, Ukristo umebadilika sana, katika siku hizi za mwisho. Sasa inakubidi kumdekeza mtu, kuwapa ahadi chungu nzima, kuwapa vitu vingi, kuwafanya waamini, waje kanisani, na kuwaahidi kwamba watakuwa na marafiki bora na kadhalika. Huo sio Ukristo.

71 Ukristo si kudekezwa. Ukristo ni mgumu. Kweli. Ni—ni ninii—ninii . . . Ukristo sio mmea wa kitalu maalumu.

72 Mmea wa kitalu maalumu ni mmea chotara, mara nyingi. Inakubidi kuunyunyizia dawa wakati wote, kuukinga na wadudu. Hiyo ni kwa sababu ya udhaifu wake. Na hivyo ndivyo inavyokupasa kuwafanyia Wakristo wengi, kuwanyunyizia kwa namna fulani na a—ahadi nyingi.

73 Wewe, huuhitaji. Mmea halisi wenye afya hauhitaji unyunyiziaji wowote. Wadudu hukaa mbali nao.

74 Ni kama tu vile, leo hii, ambapo mwanadamu anajaribu kuchukua vitu na kuvipotosha. Mungu, hapo mwanzo, Yeye alisema, "Kila mbegu na izae kwa jinsi yake."

75 Nilikuwa nikisoma kwenye *Readers Digest* hapa, ambapo wao—wanachukua kile kinachoitwa mhindi chotara, nao hufanya suke lililo bora, hakika, suke kubwa la kupendeza; bali halifai kitu, halina chochote. Nao wanafanya nyanya iliyo bora, hata haina ladha ya nyanya, na kufanya, wana kuku sasa ambaye hata hana mabawa. Kuchanganya mbegu! Mnaona?

76 Na sasa, kumbukeni, unaweza kuwa na mhindi chotara, bali huwezi kuipanda mbegu hiyo tena. Haitazaa tena. Itakufa. Kwa nini? Haina uhai ndani yake. Huna budi kuichanganyishia mbegu kila wakati. Kama sivyo, ingeendelea tu kuzaana. Hiyo inaonyesha kwamba mageuzi ya kimaumbile, kulingana na mawazo ya mwanadamu, si sahihi.

77 Unaweza kumchukua fa—farasi jike na punda dume, na kuwazalisha pamoja na kupata nyumbu, bali nyumbu hawezi kuzaa tena nyumbu mwingine. Amekwisha. Hivyo tu. Amekwisha.

78 Nao wanasema sasa, kwamba katika miaka mingine ishirini, wasipowazuia watu hawa kula hivi vitu vilivyochanganywa mbegu, kama ya mhindi na ngano na vitu wanavyozalisha kichotara, kwamba, "Kunabadilisha ha—hali ya wanawake. Hawataweza kujifungua watoto, katika miaka ishirini kuanzia sasa. Kunaua uzazi." Hakuna chochote ndani yake.

79 Wanadamu hawajaumbika kama walivyokuwa hapo awali. Mwangalie mwanadamu siku hizi. Mbona, wao, ilikuwa kwamba, michezo ya mpira ilikuwa migumu. Sasa inawabidi kuvaa kofia za chuma; wanaua dazani moja kila mwaka, wakipiga vichwa vyao kama kanga, anakufa sasa hivi; mapigano na kadhalika. Mwanadamu ameumbwa na lundo la takataka. Ni, na ni kwa sababu ya vitu chotara, na hiyo imechafua mfumo wote wa—wa maisha yetu, kanuni zote za maisha yetu.

80 Na—na—na huko kuchanganya mbegu kumeingia kanisani, pia. Badala ya kuwa na kundi halisi la waaminio wagumu wa Biblia, wameifanya chotara kwa madhehebu. Na inawabidi kuwa, "Niko na *hiki*, niko na *kile*; na mimi ni mfuasi wa *hili*, na ni mfuasi wa *lile*." Ni chotara, na kitu hicho hakiwezi kujizaa tena.

81 Tunahitaji Kitabu cha Matendo tena. Lakini njia pekee utakayofanya hivyo ni kurudi kwenye Biblia, na mbali na baadhi ya hii dini chotara.

82 Kuchanganya mbegu, lazima udekezwe! Hamna imani! Bonge tu la—la manyoya, waliofanywa dondoa dume, wakaingizwa kwa kudekezwa. "Mimi ni . . . " Nasema, je! wewe ni Mkristo? "Mimi ni Mmethodisti." Je! wewe ni Mkristo? "Mimi

ni Mpresbiteri. Mimi ni Mpentekoste." Hiyo haimaanishi *hilo*, kwa Mungu. [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.]

83 Wewe ni Mkristo kwa sababu umezaliwa katika Roho wa Kristo, nalo Neno la Mungu linaishi ndani yako.

84 Mnajua, mimi daima ninamfurahia farasi wa mbegu njema. Mwajua, huyo ana ufahamu. Unaweza—unaweza kumfundisha mambo, kumfanyia mambo, naye atajifunza. Lakini ukimchukua maskini nyumbu, huwezi kumfanyia chochote. Yeye ni maskini punda mkubwa mwenye masikio marefu. Anaketi hapo, na, ungeweza kuzungumza naye, atayainua masikio yake, na, "Hoo? Hoo? Hoo?" Mnaona, huyo, yeye ni chotara tu.

85 Inanikumbusha, wengi wa hawa wanaojiita Wakristo, chotara, dini ya punda. Unawaambia Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele; anasema, "Siamini Hilo." Mnaona? Na kwa hiyo huwezi kumfundisha chochote. Unawezaje kumfundisha; huyo amekwisha, kwa vyovyote. "Kanisa langu linaliamini *hivi*. Langu linaliamini Hilo kwa njia *ile*." Bali Neno la Mungu linasema Yeye ni yule jana, leo, na hata milele! Simpendi Mkristo wa mbegu iliyochanganywa.

86 Ninapenda—ninapenda farasi wa ukoo safi. Anajua baba yake ni nani, mama yake ni nani, ni nani babu yake na nyanya yake. Anajua vizazi vyote kotekote huko nyuma.

87 Vivyo hivyo na Mkristo wa ukoo safi, anajua ni Nani aliye Baba yake. Anatoka kwa Mungu; Yeye ni Neno la Mungu, Yeye ni yule yule kama alivyokuwa daima. Yeye ni mzao halisi wa ukoo safi wa Mungu, Neno la Mungu liko ndani yake, Yesu Kristo akijidhihirisha Mwenyewe.

88 Kundi la wasioamini! Yesu alitaka kuondoa kundi la wanyonyaji siku moja, alikuwa na wengi sana wakimfuata. Alikuwa na wanafunzi Wake. Halafu, alikuwa na wale sabini, shirika la wahudumu. Halafu, alikuwa na kusanyiko, maelfu. Ndipo akatoa tamshi hili, akasema, "Msipoila Damu... msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake, hamna Uzima ndani yenu."

89 Sasa unafikiri daktari wa tiba angesema nini, akiwa ameketi huko kwenye kusanyiko? Unafikiri mtu mwenye mawazo ya busara angesema nini, yale tunayoita mawazo ya busara? Kamwe hakulielezea. Haikumbidi kulielezea. Mbona, daktari angesema, "Achaneni na Jamaa huyo. Yeye ni mwendawazimu. Yeye... Tutakuwa vizuu wafyonza damu ya watu. Kunywa Damu ya Mtu, kula mwili Wake?"

90 Nalo kusanyiko, ningewazia kuhani alisema, "Huu ndio wakati. Hapa ndipo tunapoingilia. Haya twende! Hatutahudhuria mwingine wa mikutano hiyo." Wakaenda zao. Basi, aliwaondoa wote kutoka Kwake.

91 Ndipo akageuka na kuwaambia wale sabini, akasema, “Mtasema nini mtakapomwona Mwana wa Adamu akipaa juu kwenda Mbinguni alikotoka?”

92 Sasa, hao sabini walisema, “Mwana wa Adamu akipaa juu kwenda alikotoka? Mbona, tumekuwa Naye kwenye hori yenyewe alimozaliwa. Tunamjua mama Yake. Tumeona nguo, nguo za kitoto alizofungiwa. Alizaliwa huko chini katika Bethlehemu ya Yuda. Alilelewa huku Nazareti. Hao hapo ndugu Zake, dada Zake, na wote hao pamoja nasi. Ndipo basi Yeye akasema, ‘Huyu Mwana wa Adamu alipaa juu?’” Sasa, hakulieleza, Yeye alilisema tu. Sasa, wasingeweza kulielezea, wasingeweza kulifahamu mioyoni mwao. “Vema,” walisema, “hapa ndipo tunapoingilia,” kwa hiyo wakaondoka. Hicho ndicho kiasi kile walichoweza kustahimili.

93 Wangali wana makundi yayo hayo. Hiyo ni kweli. Tungali nao. Tunatambua.

94 Kisha akageuka. Kumbukeni, hao wanafunzi wasingeweza kuelezea hilo, pia, bali walikuwa na imani. Ndipo Yesu akageuka na kuwaangalia wale kumi na wawili, na kusema, “Je! nyinyi pia mtaondoka?”

95 Ndipo Petro akatamka yale maneno maarufu, “Bwana, twende wapi? Kwa kuwa tumeshawishika kabisa, tunajua kwamba Wewe unalo Neno la Uzima, na Wewe pekee.” Mnaona? Wasingeweza kuelezea jinsi walivyokuwa wanaenda kula Mwili Wake na kunywa Damu Yake. Wasingeweza kuelewa jinsi alivyokuwa anaenda kupaa juu kutoka kule alikoshuka kutoka, wakati alizaliwa Bethlehemu. Wasingeweza. Lakini, unaona, imani haijui kushindwa. Imetia nanga. Inadumu pale, haijalishi kile chochote kimesema. Ilidumu pale. Walikusudiwa Uzima huu. Na Yeye ni . . . Walidumu pale.

96 Sasa hao wa aina mbalimbali. Wengine waliamini. Wengine walisema, “Hakuna mtu aliyewahi kunena hivi.” Wengine hawakuamini, nao wakasema, “Loo, hilo, huenda walizungumzia hilo.”

97 Wengine wakasema, “Hakuna mtu aliyewahi kunena kama Mtu huyu. Kuna kitu cha ajabu kumhusu. Kile asemacho, Yeye anaweza kukitimiza.” Vema, walisema kwamba, unajua, walisema, “Yeye hazungumzi kama kuhani. Hazungumzi kama rabi. Kwani yale asemayo, Mungu huyaunga mkono, huthibitisha yale aliyosema Yeye.” Loo, jamani!

98 Hapana shaka ilikuwa ni kijana Yohana, wakati huo, alisema, “Wazieni hilo! Tunaye pamoja nasi hivi sasa. Ni faraja jinsi gani hiyo! Ni usalama jinsi gani!” Ni usalama jinsi gani unaopaswa kuwa kwetu!

99 Mimi ni mmishenari, kuzunguka na kuzunguka ulimwengu. Nami nimeona kila namna ya dini na kila namna ya miungu walio nao, miungu wa kikafiri; Waislamu, Budha, na

Makalasinga, Jaini, loo, chochote kile, na miungu wa kikafiri wa makabila. Lakini, kila moja ya hizo, hakuna moja iliyo ya kweli ila Ukristo. Kila moja ya hizo, waanzilishi wao wamekufa, nao wana kaburi alimozikwa. Bali Ukristo ndiyo ya pekee iliyo sahihi, kwa sababu Mwanzilishi wetu alikufa, akazikwa, lakini alifufuka tena, nasi tunaweza kuthibitisha kwamba Yu hai.

100 Kwenye kaburi la Muhammed, kwa miaka elfu mbili iliyopita, karibu hiyo, kumekuwa na farasi mweupe, wakibadilisha walinzi baada ya kila saa kadhaa, wakimngojea Muhammed kufufuka kutoka kwa wafu na kumpanda farasi na kuingia ulimwenguni na kuuteka.

101 Lakini Yesu tayari ametoka kwa wafu, amekuwa hai kwa miaka elfu mbili, na yu pamoja nasi usiku wa leo. Halafu basi tunapoona giza, na kuona mwisho wa wakati, jinsi ulivyo sasa, kufikia saa hizi tunazoishi, tunaposafiri kwenye bahari ya kawaida ya maisha, ambapo bahari zenye dhoruba, na—na chombo kinaweza kuzama wakati wowote. Taa hizi ndogo zinaweza kuzimika upesi namna *hiyo*. [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] Ama, huenda tusiondoke kwenye jengo hili usiku wa leo, si hata mmoja wetu. Hatujui ni wakati gani mauti yanapokuja.

102 Na ni hisia ya usalama jinsi gani iliyokuwa bila shaka, kwa hao wanafunzi, kujua ya kwamba Muumba mwenyewe, ambaye alikuwa amejitambulisha Mwenyewe kikamilifu kuwa ni huyo Mtu, alikuwa anasafiri pamoja nao.

103 Na jinsi lilivyo wazo lenye baraka, ni tumaini lenye baraka jinsi gani, ni uhakika wenye baraka jinsi gani, katika saa hii yenye giza kwenye mwisho wa historia ya ulimwengu, kujua kwamba Muumba anasafiri kwenye bahari ya kawaida ya maisha pamoja nasi, tuko salama ndani! Mabomu, chochote kiwezacho kuja, acha waendeshe, wapasue, walipue, chochote watakacho, haileti tofauti yoyote kwangu mimi, ninasafiri pamoja na Muumba. Ni usalama jinsi gani, huku nikisafiri kwenye maji haya!

104 Sasa wakati wakizungumza, wakiongea juu Yake, kuhusu mambo makuu aliyokuwa amefanya. Baada ya karamu ya uamsho, Yesu alikuwa labda anapumzika kama anavyopumzika, nilisema, katikati ya miamsho. Ndipo sisi...walikuwa wametambulishiwa wazi sana kuwa Yeye ni Nani. Watu walijua kuwa Yeye ni Nani, kati ya wale aliokuwa akiwapofusha. Lakini wale walioyashika Maandiko, kwa kuwa walifahamu kwamba Maandiko...Neno la Mungu limetolewa, sehemu, kwa kila kizazi, na ahadi hiyo ya wakati huo haina budi kutimizwa. Naye alitimiza hasa kile kilichopaswa kutimizwa katika wakati wa Masihi. Alitimiza kila sifa. Ndipo sisi...alihakikishiwa kwamba Yeye alikuwa Ndiye.

105 Lakini, mnaona, Yeye alikuwa ni wa kawaida sana. Hakuvalia kama kuhani. Alikuwa, hana, hana elimu kwa—kwa kile ambacho tungekiita elimu. Hatuna ushahidi ulioandikwa wa Yeye kwenda shule hata. Bali kulikuwa na jambo kumhusu ambalo lilikuwa ni tofauti.

106 Halafu basi akawaalika, wakati wasingeweza kuelewa, kasema, "Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Yanawaambia kuwa mimi ni Nani."

107 Na sasa, kumbukeni, wote walikuwa na hii moyoni mwao na walikuwa wakiwazia mambo haya. Na wakati wakisafiri huku baharini, jinsi wangekuwa kama watoto, mradi tu alikuwa kwenye mashua pamoja nao.

108 Sasa, ewe rafiki, kile jambo hilo linachopaswa kutufanyia sisi! Yesu Kristo yeye yule aliyetambulishwa, Muumba yeye yule, Mungu yeye yule, yu pamoja nasi usiku wa leo. Jinsi i—ilivyo salama, hisia ya jinsi gani, kujua kwamba Uwepo Wake upo hapa.

109 Sasa tunaona, papo hapo walipokuwa na wakati huu wa ajabu, mara ghafla, shida ikainuka. Merikebu ikasukasukwa, matanga yakapasuka, maji yakaijaza mashua. Matumaini yote ya kunusurika yakaisha.

110 Sasa, si ni ajabu, kama tu ilivyo sasa, tunavyokuja kwenye mwisho sasa, si ni ajabu? Tunaweza kuzungumzia jinsi alivyo mkuu; tunaweza kusema jinsi alivyo mkuu, kanisani mwetu tunapotoa ushuhuda; tunawaambia wa—waajiriwa wetu, waajiri, jinsi alivyo mkuu; tunawaambia watu mtaani jinsi alivyo mkuu; na, shida inapotokea, tunafadhaika. Mnaona? Tunaninii tu . . . Mnaona? Mambo ambayo tumemwona akifanya, mambo tunayojua kuwa Yeye hufanya; na halafu hebu ugonjwa kidogo, au shida ndogo iingie nyumbani, angalieni kinachotokea; tunachanganyikiwa kabisa, matumaini yo—yote yamekwisha.

111 Ingawa walikuwa wamemwona akifanya mambo mengi sana; yote yanasahaulika wakati shida ikiingia.

112 Kama vile sasa, tumeuona uamsho huu mkuu, tunayo historia ya miamsho mingine mikuu, tunao Uwepo Wake, tunayafahamu mambo haya, na wakati mwingine shida inaingia tusiyoweza kutatua. Wao . . .

113 Kwa mfano kama sasa, tuna shida makanisani mwetu sasa. Tuna matatizo ya kidhehebu, mabishano makanisani mwetu. Hatujui ni nini kitakachotokea. Tunaona kitu kikubwa kikiumbika huko juu. Sisi sote waaminio wa Biblia tunaona kitu fulani kinajitayarisha kutukia. Hakuna mtu ila anayefahamu hilo.

114 Nayo makanisa yote yanaenda kuingizwa katika lile Baraza la ekumeni la Makanisa. Ndipo, mtakapofanya hivyo,

mtapoteza mafundisho yenu makuu ya kiinjilisti ya Biblia. Nao Wapentekoste wanalitetea, wanaingia moja kwa moja ndani yake, kama nguruwe anayeingia machinjioni mwake, hiyo ni kweli, baraza la ekumeni. Viongozi wengi mashuhuri wa Kipentekoste wanakubaliana nao. Nawambieni, kamwe msiingize shingo yenu katika kitu kama hicho. Hicho hakika ndicho Biblia ilisema kitakuja kutimia. Huyo hapo mnyama na alama, na, kikamilifu, kila kitu kimekaa sawasawa kabisa, nasi tunaona haya na tunashangaa ni nini kitakachokuwa matokeo yake.

115 Matatizo yakaingia. Ndipo wakasahau kwamba Yule hasa waliyekuwa wakinena habari zake, Muumba mwenyewe, alikuwa kwenye merikebu pamoja nao.

Sasa unasema, "Laiti ningaliweza kuwazia hilo!"

116 Vema, kumbukeni, tungali Naye, maana Yeye ni Neno, daima. Katika Yohana 1:1, kama tulivyonena jana usiku, "Yeye alikuwa ni Neno; nalo Neno likafanyika mwili likaishi katikati yetu." Nasi tungali tuna Neno Lake ambalo hutuelekeza kwenye mawazo Yake na matendo Yake kwa ajili ya siku hii. Mnaona? Ninii . . . Si mawazo aliyokuwa nayo Musa katika siku yake, si mawazo ya wanafunzi, si mawazo ya Luther, au Wesley, au wakati wa Kipentekoste, ama wowote wa hizo. Tunayo Biblia hapa inayotuambia kuhusu kinachoenda kutukia sasa. Mnaona? Tunauona uamsho wa Kipentekoste katika Biblia, wa Kilutheri, na nyakati hizo zote za kanisa. Tuliziona. Bali pia tunayo Maandiko hapa yanayotuambia kile kinachoenda kutukia sasa. Na huyo ni Mungu, Mungu akilifasiri Neno Lake Mwenyewe kwa ajili ya wakati huu tunaoishi. Yeye hujifasiria Mwenyewe. Na, hata hivyo, tunafadhaika. Msifadhaike.

117 Wanafunzi wake wakati mwingine huingia katika matatizo ya kimwili wasiyoweza kutatua, kama vile ugonjwa, kansa, kadhalika, ambayo madaktari hawawezi, hawajui la kufanya kuyahusu. Sisi, kama wao, humsahau Yule aliye ndani ya merikebu.

118 Walipaswa kujua kuwa Yeye aliyajua mambo haya yote. Alijua kuwa yalikuwa yanenda kutokea. Alikuwa ndiye . . . Yeye aliyajua mambo yote, kwa hiyo alijua haya yalikuwa yanaenda kutokea. Hayo yakienda kutendeka kwao. Ni kwa nini Yeye aliyaacha hayo yatendeke? Alipoingia ndani ya merikebu hiyo, Yeye alijua hayo yalikuwa yanaenda kutokea.

119 Alijua kwamba ilitubidi kukutana na hali hii, Naye ametutabiria hapa katika Biblia ingekuwa hivyo.

Sasa Yeye alikuwa anafanya nini? Kuijaribu imani yao.

120 Ni kwa nini angemwacha ma—ma—maskini mwanamke mzuri anayeonekana kuwa ni mama kuketi kwenye kiti cha magurudumu, namna hiyo? Ni kwa nini angewaacha jamaa wadogo wazuri hapa, hawa vijana wanaume wanaoketi hapa

kwenye viti hivi vya magurudumu, kina mama, na kadhalika? Kwa nini afanye hivyo? Na, hata hivyo, huenda wamelemaa, wanaishi tu maisha ya kawaida. Bali huenda kukawa na wengine wameketi hapa na matatizo ya moyo, na, Mungu asipokuponya, huenda ukafa kabla ya asubuhi. Hiyo ni kweli. Alijua lilikuwa linaenda kutokea. Labda imefanywa ili kujaribu imani yetu. Hiyo ndiyo sababu lilifanywa kwa ajili yao. Alisema hivyo. Mnaona? Vivyo hivyo sasa.

121 Alikuwa amethibitisha kuwa Yeye ni Nani, kwa Maneno na ishara alizokuwa amethibitisha miongoni mwao, kwamba alikuwa ndiye Masihi mtiwa mafuta aliyethibitishwa, aliyekuwa yuaja.

122 Naye amethibitishwa miongoni mwetu, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu na kurudi kwa mambo yale aliyoahidi katika siku hii, kwamba Yeye angefanya. Amethibitisha kwamba yupo hapa. Anathibitisha kwamba ni yeye yule, jana, leo, na hata milele. Basi mnaona jinsi tunavyoweza kufadhaika kwa urahisi kwenye jambo lolote dogo? Hatupaswi kuacha hilo litendeke. La.

123 Alisema, "Kama sizitendi kazi zilizoandikwa kunihusu, basi msiniamini Mimi." Na iwapo Kanisa, iwapo Roho Mtakatifu leo, hatendi yale mambo aliyopaswa kutenda kwa majira haya, basi msiamini Ujumbe; mnayo haki ya kutokuamini Huo.

124 Lakini Yeye aliahidi kwamba mambo haya ambayo Yeye anafanya hivi sasa yangefanyika moja kwa moja kwenye wakati huu. Kwa hiyo linapaswa kutufanya tujisikie salama sana, tuseme, "Ninapanda kwenda kwenye mkutano. Roho Mtakatifu mkuu, ninasikia, yuko kule juu akizifunua siri za mioyo ya watu." Hilo ndilo hasa alilosema angefanya wakati Yeye atakapofunuliwa katika siku za mwisho. Yesu Kristo alisema, Mwenyewe, kwamba hilo hasa ndilo Yeye angetenda.

125 Tena akasema, "Ulimwengu utakuwa katika hali kama ulivyokuwa katika siku za Sodoma." Hapo tu ndipo ulipo sasa. Alisema, "Makanisa yatatengana, kama tu yalivyokuwa wakati ule," Lutu, aliye vuguvugu, huko chini Babeli, ama huko chini Sodoma, na Wasodoma. Alisema, "Ibrahimu, kundi teule, lililoitwa litoke," na Yeye alimtuma mjumbe kwa kundi teule. Pia akawatuma wajumbe wawili huko chini kwa hao, kuwakilisha kila mmoja. Na hilo hasa ndilo ambalo amefanya, hata kwa kila jina, kila tendo, kila msogeo, kila kitu kikamilifu tu, kila ishara, kila dhihirisho, sawa tu kabisa. Alisema lingefanyika.

126 Sasa tunatishwa na nini? Haya mambo yako juu yetu kwa nini? Yeye anatujaribu, kuona kile tutakachofanya kulihusu. Tazama.

127 Aliwaambia, kasema, "Sasa, kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi nizifanyazo; zinashuhudia kuwa Mimi ni nani." Walipaswa kulijua, bali hawakulijua. Wao . . .

128 Yeye alikuwa ni Mungu, Yule aliyeumba, Muumba wa upepo na bahari. Kama aliweza kuumba upepo na bahari, si angeweza zaidi kuzifanya zitii Neno Lake? Kama aliumba kila kitu, si anaweza kufanya kila kitu kutii? Hebu tukumbuke, pia, aliumba miili yetu, hiyo pia itabidi itii Neno Lake. “Vema,” unasema, “kama ningaliweza tu kuwa na hakika na hilo.” Vema, tuna hakika nalo. Yeye yupo hapa kulithibitisha hivyo. Haina budi kulitii. Kumbuka. Yeye anayo . . .

129 Wakati tumelala, labda si chochote ila kijiko kimoja tu cha majivu, Yeye aliahidi kufufua hayo majivu. Aliahidi kufufua hayo. Mwili hauna budi kumtii. Na hapo ni wakati tunapokufa, tuna hakika kwamba tutafufuliwa, kwa kuwa Yeye aliahidi atafanya hivyo. Nayo ahadi Yake ni Neno Lake, nasi tunaamini. Mnaamini katika ufufuo wa mwili? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hakika. Kama huamini, wewe si Mkristo. Kwa hiyo tunaamini kwamba Yeye atatufufua katika siku za mwisho. Aliahidi kufanya hivyo. Basi hilo ni nini? Hilo ni Neno Lake. Hapo ndipo tunapotumainisha kila kitu tulicho nacho, moja kwa moja kwenye hilo Neno.

130 Ndipo basi inapofikia wakati ambapo tunaliona hilo Neno likitambulishwa, kuwa pamoja nasi; basi tuko kama wanafunzi, katika kisa kingine walipokuwa huko nje baharini, na—nao walikuwa karibu kuzama tena, kwenye tukio jingine. Ndipo wakamwona Yesu akija akitembea juu ya maji, nao wakaogopa. Wakasema, “Ni—ni mizuka. Inatisha.” Walihofia kwamba ilikuwa ni pepo, nao wakalia kwa hofu. Kitu cha pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, walikiogopa.

131 Na ndivyo ilivyo leo, kitu chenyewe cha pekee kinachoweza kuwasaidia watu, wanakiogopa. Akasema, “Msiogope. Ni Mimi.” Ananena. Ungejuaje ilikuwa ni Yeye? Yeye hutambulishwa kwa Neno Lake. Hivyo ndivyo alivyotambulishwa mara ya kwanza. Hivyo ndivyo anavyotambulishwa kila wakati, kwa Neno Lake. Tazama.

132 Baada ya hawa wanafu-. . .wanafunzi kujikuta kwenye mwisho, hapana shaka baadhi yao walianza kufahamu ya kwamba Muumba alikuwa angali pamoja nao.

133 Natumai ndivyo inavyotufanyia, usiku wa leo, kwa kuwa Waebrania 13:8 inasema ni Yeye yule.

134 Basi walifanya nini? Walimwamsha Yesu. “Nenda kamwamshe Yesu. Mwamshe, mwite jukwaani!” Yeye huitwa kwa urahisi sana. Walikuwa wameona, kuona mambo mengi sana ambayo Mungu alikuwa amefanya, na—na—nayo Maneno yakimthibitisha. Nasi pia. Na haikuwa vigumu kumwita aingie kazini.

135 Walimwamsha, na kusema, “Je! Wewe. . .Wewe hujali kwamba sisi tunaangamia?”

Mnasema, “Tunawezaje kuwa na hakika na jambo hili? Je! tunaweza kulithibitisha?”

136 Yohana 14:12, Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Hiyo ni hakika. Imani yetu ikimleta Kristo mbele zetu.

137 Yeye alisema katika—katika Luka, mlango wa 17, “Katika siku za mwisho atakapofunuliwa Mwana wa Adamu, utakuwa ni wakati kama Sodoma na Gomora.” Tunaona hilo likitendeka.

138 Alisema, kabla ya wakati huo kutokea, katika Malaki 4, kwamba, “Kutakuwa na Ujumbe utakaotokea utakaowarudisha watu kwenye Imani asili iliyotolewa mara moja kwa watu.” Daima mpango wa Mungu kutenda hilo. Ndipo basi waovu watakuwa majivu, nao wenye haki watatembea juu ya miguu yao.

139 Tunaona haya yote yameahidiwa. Yeye anakungojea sasa hivi, wewe, wewe, kila mmoja wenu, kumwita jukwaani. Kumwita jukwaani! Hapo ndipo anapotaka kuwa, aitwe kwenye jukwaa la tendo. Angalia wakati ukimwita jukwaani, ndipo basi tungesema, “Hebu tumwamshe.” Halafu, mwite athibitishe Neno Lake na ja—jambo aliloahidi kutenda, jinsi angefanya. Tungejua, katika kufunuliwa kwa Yesu Kristo katika siku za mwisho, itakuwa kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma. Aliahidi ufunuo huo kwa Kanisa, wakati atakapofunuliwa. Kwa hiyo usitilie shaka na kuogopa, ni Yeye yule jana, leo, na hata milele.

140 Nilimsikia mwanamke, wakati mmoja, wakati nilipokuwa nikizungumza kuhusu Yeye kuwa ni mkuu sana. Akasema, “Kuna kitu kimoja nilicho nacho kinyume na mafundisho yako, Bw. Branham.”

141 Nikasema, “Vema, asante, ikiwa una jambo moja pekee.” Nikasema, “Na—natumai Mungu analipata tu hivyo.” Ndipo akasema, “Vema, wewe hujivuna kupita kiasi juu ya Yesu.”

142 Nikasema, “Natumai hicho ndicho kitu pekee dhidi yangu.” Ki—kisha nikasema, “Sijivuni vya kutosha juu Yake.”

143 Akasema, “Loo, naam, unajivuna.” Kasema, “Unamfanya Mungu.” Ilikuwa ni mwanamke ambaye hakuamini kwamba Yesu alikuwa ni Mungu. Alikuwa wa Sayansi ya Ukristo. Ndipo kasema, “Unamfanya Yeye—unamfanya Yeye Mungu, unamfanya Yeye Mungu.”

144 Nikasema, “Ama Yeye ni Mungu, au mdanganyifu mkubwa kuliko wote ulimwengu uliowahi kujua.” Nikasema, “Yeye . . . ”

145 Kasema, “Vema, ninaweza kukuthibitishia, kwa Biblia yako, kwamba hakuwa Mungu. Yeye alikuwa tu ni nabii.”

Nikasema, “Alikuwa nabii, kweli, lakini alikuwa Mungu, vile vile.”

Kasema, "Yeye alikuwa ni mwanadamu na alikuwa apatikanaye na mauti."

Nikasema, "Hiyo ni kweli, pia."

146 Akasema, "Njiani akienda kumfufua Lazaro kutoka kaburini, Yohana Mtakatifu mlango wa 11, kasema, Biblia ilisema, 'Yesu alilia.'"

Nikasema, "Hiyo ni kweli."

147 Akasema, "Vema, hiyo inathibitisha kwamba asingeweza kuwa ni Mungu, huku analia."

148 Nikasema, "Loo, jamani, mama, hiyo ndiyo hoja yako?" Nikasema, "Hiyo ni dhaifu." Akasema . . . Nikasema, "Kweli, Yeye alikuwa ni mwanadamu wakati alipokuwa analia; bali alipoutia mwili Wake mdogo kazini, akayavuta maskini mabega Yake na kusema, 'Lazaro, njoo huku,' na mtu aliyekuwa amekufa siku nne, na alikuwa akioza kaburini, alisimama kwa miguu yake na akawa hai tena, huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu. Huyo alikuwa ni Mungu."

149 Alikuwa ni mwanadamu, hapa nje katika merikebu hiyo usiku ule, alipokuwa huko nje baharini, wakati pepo elfu kumi wa baharini walipoapa kwamba wangemzamisha. Maskini merikebu hiyo ndogo ikasukasukwa kama kizibo cha chupa kwenye bahari yenye tufani. Alikuwa ni mwanadamu, mchovu, akilala. Lakini walipomwamsha na kumwita jukwaani, aliweka mguu mmoja demani na kuangalia juu, kisha kasema, "Amani, tulia," ndipo pepo na mawimbi yakamtii. Huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Huyo alikuwa ni Mungu.

150 Yeye alikuwa ni mwanadamu wakati aliposhuka kutoka mlimani, mwenye njaa, akiangalia mtini apate kitu cha kula. Alikuwa ni mwanadamu wakati alipokuwa na njaa. Lakini alipochukua biskuti tano na samaki wawili, na kuwalisha watu elfu tano, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Huyo alikuwa ni Mungu ndani ya mtu huyo.

151 Kila mtu ambaye amewahi kuwa wa maana, ni watu walioamini hilo. Kweli. Washairi na wengine waliamini hilo, kwamba Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akijipatanisha Mwenyewe na ulimwengu.

152 Na sasa Kristo yumo Kanisani, akiwapatanisha watu kwa Mungu. Aliahidi kufanya hivyo. Imeandikwa, kwamba, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ninaamini hilo kwa moyo wangu wote, kwamba Yeye anangojea tu sasa kuitwa jukwaani. Sasa kitu pekee kinachoweza kumwita jukwaani, ni kwamba tumwamshe ndani yetu, tumwite jukwaani.

153 Alikuwa ndiye karama kuu kuliko zote Mungu alizowahi kuzipa ulimwengu. "Mungu aliupenda sana ulimwengu hata akamtoa mwanawe wa pekee; yeyote amwaminiye hataangamia;

atakuwa na Uzima wa Milele." Mwangalie Mungu na karama Yake. Sasa, watu waliitumia karama ya Mungu.

154 Maskini mwanamke mmoja, wakati mmoja, aliamini hilo, kwamba Yeye alikuwa ni dhihirisho la Mungu katika mwili. Naye akasema, "Kama nikigusa vazi Lake, ni—ni—nitakuwa mzima."

155 Sasa, aligusa vazi Lake. Ndipo akageuka, na kusema, "Ni nani aliyenigusa? Mnaona, nguvu, uweza, umenitoka." Aligusa vazi Lake. Huyo alikuwa ni mwanamke huyo akiitumia karama ya Mungu. Mnaona? Akawa dhaifu kutokana na hilo.

Lakini wakati alipoondoka nyumbani mwa Lazaro . . .

156 Kumbukeni, Yohana Mtakatifu 5:19, Yesu alisema, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile ambalo amwona Baba analitenda." Kumbukeni, Yesu Kristo kamwe hakutenda mwujiza mmoja, hakutenda lolote kwa njia ya kimbinguni, isipokuwa kwanza aliona ono juu ya jambo la kufanya. Ni wangapi wanaamini hilo kuwa ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yohana Mtakatifu 5, "Amin, si lile ninalosikia, si lile mtu mwingine analoniambia; lile nimwonalo Baba analitenda, hilo atenda Mwana pia." Sasa kama hilo sivyo, basi Maandiko mengine yote si kweli. "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe; ila lile ambalo amwona Baba analitenda, hilo atenda Mwana. Baba afanya kazi, nami nafanya kazi mpaka sasa." Kwa maneno mengine, Yeye aliweka tu katika matendo, kufanya yale Mungu alimwambia afanye.

157 Sasa, kumbukeni, alipoondoka nyumbani mwa Lazaro, alikuwa ameenda siku kadhaa. Lazaro akawa mgonjwa, nao wakaagizia aitwe. Hakuenda. Siku mbili baadaye, Lazaro akawa mgonjwa zaidi. Kwa hiyo wakaagizia aitwe tena, bado hakuenda. Ndipo wakati uliokusudiwa, Baba alikuwa amemwonyesha lingetokea, Lazaro akafariki. Ndipo akageuka, wakati Lazaro alipokufa, kasema, "Lazaro amekufa, nami nina furaha kwa ajili yenu sikuwapo." Wangekuwa wanamsihi amwombee, na kadhalika. Alifanya tu lile Mungu alilomwambia kufanya, lile aliloona, ono. Mnaona, alikuwa ameona ono juu ya jambo la kufanya. "Bali ninaenda kumwamsha." Hmm! Haya basi.

158 Mwangalie Martha akija kumwona. Alisema, "Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa." Mnaona?

159 Yeye alijua kile alichokuwa anaenda kufanya. Mwangalie kwenye kaburi la Lazaro. Alisema, "Baba, nakushukuru Wewe, Wewe umenisikia tayari, bali nilisema tu hilo kwa ajili ya hawa wanaosimama karibu."

160 "Lazaro, njoo huku!" Ndipo Lazaro akafufuka kutoka kwa wafu.

161 Sasa, kamwe hakusema chochote kuhusu kuwa dhaifu pale. Huyo alikuwa ni Mungu akitumia karama Yake. Na watu wakitumia karama ya Mungu ilikuwa tofauti.

162 Kwa kuwa, Yeye alikuwa ni Neno. "Nalo Neno ni kali kuliko upanga ukatao kuwili," Biblia inasema, "na huyatambua mawazo na makusudi ya moyo." Hilo linathibitisha kwamba Mungu yu miongoni mwa watu. Naam. Hebu na tuliamini. Yeye yuko tayari, kulingana na Neno Lake, kuitwa jukwaani, usiku wa leo.

163 Ni wangapi waliopo hapa wagonjwa na wahitaji, inueni mikono yenu. Hebu tuione mikono yenu, ni wangapi walio wagonjwa na wahitaji, popote. Vema, kitu cha pekee anachongojea ni kuitwa jukwaani. Mwombe tu.

164 Sasa vipi kama Yeye angalikuwa amesimama hapa amevaa suti hii aliyonipa, nawe uje mbele Zake na kusema, "Bwana Yesu, ninataka uniponye," unajua kile angesema? "Nimekuponya tayari."

165 "Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Hawezi kufanya hivyo mara ya pili. Kwa hiyo, unaona, amekuponya tayari. Inakubidi kuliamini. Hakuna kitu uwezacho kufanya, cha kustahili chochote, ku—kustahili wokovu wako au uponyaji. Hakuna kitu uwezacho kufanya kuuhusu. Ni kipawa cha Mungu cha bure. Unaona, ni neema, kipawa cha bure. Kama nikikupa dola milioni moja na kisha uinyooshe tai yangu; sikukupa; ulizifanyia kazi. Unaona? Kipawa cha Mungu ni cha bure. Jambo la pekee unalopaswa kufanya ni kuamini, kwamba Yeye amekununulia hiki, wewe. Yeye. . . Kimenunuliwa tayari. Alikufanyia hilo. Wala hakuna mtu duniani. . .

166 Sijui ni nini mmekuwa nacho hapa Baton Rouge. Kila kitu kinaisukumia nchi, uigizaji na hayo. Tunajua hayo sharti yawe hivyo. Lakini mtu anapoingia na kukuambia kwamba ana uwezo kukuponya, huyo anasema uongo. Mungu pekee aweza kuponya. "Mimi ni Bwana Mungu wako ayaponyaye magonjwa yako yote." Kamwe hataushiriki utukufu Wake na yeyote. Hakuna mtu aliye na uwezo kuponya.

167 Ila kuna watu walio na karama, kumdhihirisha Mungu. Mchungaji wenu. . . [Ndugu Branham anakohoa—Mh.] Samahani. Anaweza kumchukua Mungu, kwa karama ya—ya. . . Mwalimu, yeye anaweza kulielezea Neno hata inakubidi kuliona. Iwapo una macho yoyote ya kuona, utaliona. Ipo nyingine, labda karama nyingine. Bali daima kuna karama inayodhihirisha Uwepo wa Mungu, na, kupitia hapo, wewe mwenyewe huna budi kuiamini.

168 Mwenye dhambi anaweza kuja hapa kwenye madhabahu kama kijana mwanamume au msichana, kwenye umri wa miaka kumi na minne, na wangekuletea chakula chako hapa,

nawe ungemlilia Bwana, mpaka uwe na umri wa miaka tisini, kamwe usingeokoka. Ila kwanza inakupasa kukikubali kile alichokufanyia. Unaona? Huna budi kukikubali, wewe mwenyewe. Ndipo unapokikubali, basi Yeye ni Kuhani Mkuu, mpatanishi, kufanya maombezi juu ya maungamo yako ya kile unachoamini.

169 Sasa hilo ni jambo lile lile na karama kwa njia hii. Ni kuweka nia yako mbali na wewe, ndiposa uone kile anachosema ufanye.

170 Ninawaona watu wakija mimbarani, wanarukaruka na kupiga mayowe, na kusema, "Loo, Ndugu Branham, nina imani yote ulimwenguni." Unafanya nini hapa juu, basi? Mnaona? Huo—huo ni mhemuko, wala si imani.

171 Imani halisi haijui kushindwa. Imefanyika tayari. Imekwisha tayari. Mungu alisema hivyo, na hilo latosha, unaona. "Mungu alisema hivyo!" Sasa ni kitu kile kile, wakati wowote. Wakati ukiliamini kweli, hiyo inamgusa.

172 Sasa maskini mwanamke yule aliyeligusa vazi Lake, alisema, "Kama tu nikigusa vazi Lake, nitakuwa mzima," ndipo akafanya hivyo. Na wakati alipotekeleza yale imani yake ilitaka afanye, "kuligusa," Yeye aliuhisi, unaona, ndipo akageuka na kuzungumza naye.

173 Sasa, ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ikiwa tu utamwamini tu Kristo, amini! Hebu acha imani yako iguse vazi Lake. Na Yeye, sasa hivi, ni Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Sote tunajua hilo. Na ikiwa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, itabidi Yeye atende leo kama alivyotenda jana kama Yeye ni Kuhani Mkuu yule yule. Sasa je! hamtaliamini hilo? Iweni tu na imani katika Mungu.

174 Kama nimewaambia jambo lisilo kweli, basi Mungu hataliunga mkono. Lakini nimewaambia Kweli, Yeye ata—Yeye ataliunga mkono. Anawajibika kuiunga mkono hiyo Kweli.

175 Yesu alisema, "Ninaye shahidi." Naye shahidi huyo ni Neno la Mungu, bila shaka. Kasema, "Hapo Maandiko yananishuhudia Mimi. Kama hayanishuhudii, basi msiamini." Mnaona?

176 Na kama Maandiko hayashuhudii yale ninayowaambia sasa, kwamba, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele," basi msiyaamini Maandiko. Kwa sababu, Maandiko yalisema ndivyo alivyo, na Yeye aliahidi mambo haya kwa ajili ya wakati huu wa mwisho. Kumbukeni, kwenye mwisho tu wa wakati wa Wayahudi, hivyo ndivyo alivyojifunua Mwenyewe, Masihi. Mwisho wa wa—wakati wa Wasamaria, alifanya kitu kile kile. Sasa ni mwisho wa wakati wa Mataifa. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

177 Mwamshe katika dhamira yako, mwite jukwaani, wakati tukiinamisha vichwa vyetu.

178 Baba wa Mbinguni, neno moja tu kutoka Kwako sasa litatosha. Litakuwa yote tunayohitaji, neno moja tu kutoka Kwako. Jalia watu waelewe waziwazi ni nini kimefanikishwa, kile tunachojaribu kufanya, Bwana, ni ku—ni kuwafanya wapate faida za Bwana Yesu wanayempenda na kumtumikia. Jalia wafanye hivyo usiku wa leo, Bwana. Kwa kuwa, kifo Chako hakikuwa bure. Wewe "ulijeruhiwa kwa makosa yetu, ukachubuliwa kwa maovu yetu." "Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tulipona." Ninaomba, Mungu, kwamba kila mmoja humu ndani, katika Uwepo wa Kiungu, ataelewa hili na atalipata ono, na ataponywa kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Kupitia Jina la Yesu Kristo, ninajitoa pamoja na kusanyiko hili, kwa heshima na utukufu Wake. Amina.

179 Sasa iweni na kicho kabisa, kwa dakika chache tu. Sasa neno moja tu kutoka Kwake litakuwa na maana kuliko yote niwezayo kusema, ama yote mtu mwingine yeyote angeweza kusema, kwa kuwa ni Yeye akifanya hivyo. Yeye ndiye. Yeye ndiye mtendaji, nasi tunatumaini ya kwamba Bwa—Bwana Yesu atawajalia mambo haya sasa, kila mmoja.

180 Sasa hebu tuone ni saa ngapi. Sikujua ilikuwa hivyo. Nakuambia, kutoka hapa kwa wakati ufaao, kile kitupasacho kufanya, hatuna muda wa kufanyiza mstari huu. Hebu tuite moja kwa moja kutoka kwa wasikilizaji.

181 Sasa hebu tuchukue tu Maandiko, kwa muda mfupi tu. Sasa Biblia inaahidi, katika siku hii, kwamba marudio ya Sodoma na Gomora yatarudiwa. Ni wangapi wanaoamini hilo sasa, inua mkono wako? Biblia inatambulisha hilo sasa.

182 Halafu basi kilikuwa ni kitu gani kile katika Sodoma na Gomora? Kilikuwa ni Mungu katika umbo la mwanadamu. Na vile ambavyo Ibrahimu alilijua hilo, ni hapo aliposema, "Ni kwa nini Sara akacheka hemani, huko nyuma? Ama, mbona aliyatilia shaka, maneno aliyokuwa amesema kuwa ndivyo?" Yeye aliweza kutambua kile Sara alichokuwa akiwazia, nyuma Yake. Sasa ninyi angalieni tu kama haikuwa hivyo.

183 Sasa, hilo halikuwa kwa kanisa la Babeli, au kanisa la Sodoma. La, la. Hilo halikuwa ni kwa ajili ya hao watu huko chini katika tabaka la kimadhehebu. La, bwana, kamwe haliwaendei. Wanaye mjumbe wao. Mnaona?

184 Bali kwa Kanisa teule, Uzao safi wa Ibrahimu unaopaswa kuliamini Neno haidhuri hali zikoje, "Ibrahimu aliviita vitu visivyokuwepo kama vilivyokuwepo." Mungu alisema hivyo, naye akaliamini. Sasa, rafiki, na—najua kwamba Mungu anawajibika kwa Neno hili, kulitimiza.

185 Sasa ninawatakeni, popote ulipo katika jengo, kuketi kwa kicho kwa dakika chache, popote ulipo. Na uamini, amini tu kwa moyo wako wote.

186 Sasa iwapo ningeweza kukuponya, iwapo ningeweza kumponya maskini msichana huyu ninayemhurumia, iwapo ningeweza kukiponya kile kitu kidogo kilicholala pale, ni—ni—ninge—ningetambaa kutoka hapa hadi Ncha ya Kaskazini, kama ningeweza, kufanya hilo, ama yeyote aliye na hisia za kibinadamu. Bali nisingeweza kufanya hilo hata kidogo. Labda baadhi yenu hapo hamtaishi ila muda mfupi tu, kwa kansa. Iwapo ningeweza kukuponya, ningekuwa. . .Nisingestahili kusimama kwenye mimbara hii kama ningaliweza kulifanya na nisingefanya hivyo. Sasa, siwezi. Moyo wangu unawahurumia. Ningalifanya hivyo kama ningaliweza, ila siwezi. Hamna mtu mwingine yeyote awezaye kufanya hivyo. Hiyo ni kweli. Lakini, mnaona, Yesu tayari amelifanya. Mnaona? Naye anajaribu tu kukufanya uamini hilo. Lakini wewe. . .

187 Ninawahurumia watu. Kumekuwako na mambo mengi sana ambayo yamewapofusha tu, *hivi* na *vile*, mpaka, maskini watu, karibu, kama kondoo wasio na mchungaji. Hawajui la kufanya. Mmoja anasema *hili*, na mwingine anasema *lile*. Usiyatafakari yale mwanadamu aliyosema. "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu."

188 Na, kumbukeni, Petro alisema, kwenye Siku ya Petekoste, "Ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, wote ambao Bwana Mungu wetu atawaita wamjie." Mnaona?

189 Yesu aliahidi mambo haya yangetokea katika siku za mwisho, kwamba Mungu angerudi katika umbo la mwili wa kibinadamu, kama mimi na wewe hapa usiku wa leo, na angefanya kazi zile zile kabla tu ulimwengu haujaangamizwa. Nao ulimwengu ungekuwa kama Sodoma. Mnaona? Sasa tunayo hali ya Sodoma hasa; kila mahali, kila mtu, kila kitu kimekaa sawa kabisa.

190 Sasa je! imani yetu haiwezi kufikia hilo? Hivi hatuwezi kumwita jukwaani? Mwiteni jukwaani. Imani yako ndicho kitu cha pekee kiwezacho kumwita. Sasa ninyi aminini kwa moyo wenu wote, kila mmoja wenu sasa.

191 Basi nataka kuwaulizeni jambo fulani. Bila kadi zozote za maombi,. . .-mwita mtu yeyote hapa juu, kama yule Roho Mtakatifu mkuu atashuka hapa, na kwa upako wako wewe na upako ulio juu yangu, na atatambulisha kwamba Yesu Kristo anafanya kazi humu miongoni mwetu namna hii, angefanya nini zaidi? Hamna ahadi nyingine katika Biblia, zaidi ya hiyo. Hiyo ndiyo ahadi kuu kuliko zote. Ni wangapi wanaojua hilo? Hakika, ndivyo ilivyo. Ndicho ki—ndicho kitu cha mwisho kwa wakati wa kanisa.

192 Wayahudi, katika wakati wa kile kipindi cha Dhiki Kuu, na kwenye. . .hapo wanako ku—kutembelewa huko nyuma, bali si kwa kanisa la Mataifa.

193 Hiki ndicho kitu cha mwisho kilichoahidiwa kwa Mataifa. Ni kweli. Mnaona, ilikuwa na Mataifa huko chini Sodoma, waliokuwa wanaenda kuteketezwa. Na huyo, huyu hapa Bi—Bibi-arusi, ambaye alikuwa ni Uzao Mteule wa Ibrahimu, akiwa ni Bibi-arusi aliyeitwa atoke miongoni mwa Mataifa. Hiyo ndiyo ishara yao ya kumalizia, yote.

194 Itie alama kwenye kitabu chako. Mimi ni mzee. Lakini wewe itie tu alama kwenye kitabu chako na uone kama itatimia, au la. Mnaona, mko kwenye mwisho sasa. Lini? Sijui. Ninamtazamia leo. Asipokuwa hapa leo, nitakuwa nikimtazamia kesho. Asipokuwepo kesho, nitamtazamia siku inayofuata. Asipokuwa hapa mwaka huu, nitakuwa nikimtazamia mwaka ujao. Ninajua Yeye yuaja. Sijui dakika wala saa, bali ninajua kila kitu kimetimizwa, tayari kwa ajili ya Kunyakuliwa. Kanisa limeitwa litoke. Kutakuwa ni kuondoka kisiri; kutoweka tu, na hayo yatosha.

195 Nao ulimwengu unaendelea tu kama kawaida, watu wakihubiri, na watu wakidhani kwamba wanaokoka, sawa tu na walivyofanya katika siku za Nuhu, kadhalika. Nuhu aliingia ndani ya safina, nao watu wakaendelea tu, na ulimwengu ukiendelea kama kawaida. Liwazie! Na, wamepotea Milele, huku wakidhani wameokoka.

196 Mojawapo ya siku hizi nitaleta hema kubwa katika nchi hii, na kulisimikisha hapa juu, kusudi tuweze kuwa na mikutano ya alasiri, na mafunzo, ili mweze kuelewa mambo haya vizuri zaidi. Tuwalete ndugu zetu wote pamoja ili tuweze kuwa na ibada.

197 Sasa kama Yesu Kristo anatimiza ahadi Yake, basi tunawajibika kumwamini Yeye. Ninawatakeni nyote, kila mmoja wenu, kuwa tu na imani rahisi ya kitoto, kumwamini Yeye.

198 Sasa wakati kwa namna fulani mnaanza huku vichwa vyenu vimeinamishwa, na mwanze kuomba, mkisema, "Bwana Yesu, sasa ninajua kwamba mtu huyu hanijui. Nami ni mhitaji. Na tunaambiwa ya kwamba Wewe ni Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Ikiwa utamruhusu tu . . . Kama ninaweza kukugusa Wewe, nena tu kupitia yeye, Bwana, kwamba nitaninii, ninajua ninii yake . . . kujua ni Wewe. Ninajua yeye hanijui."

199 Na hiyo ni huko nje kwenye wasikilizaji, kusanyiko tu lililochanganyikana; la imani, kutokuamini, imani ya kujifanya; wenye dhambi, mtakatifu, na wote pamoja.

200 Sasa lazima uamini. Sasa kama Yeye atafanya hili kutoka kwenye wasikilizaji hawa hapa, ninawatakeni kila mmoja wenu humu ndani, useme, "Ndugu Branham, na—najua hiyo ni—hiyo haina budi kuwa ni Yeye anayelitazama kusanyiko kama alivyofanya wakati ule." Ninataka wewe, kama kweli utaamini, ninataka uinue mkono wako, useme, "Bwana, nitalikubali kwa

moyo wangu wote, kwamba ninaamini ni Kristo Yesu, kulingana na ahadi Yake." Kote kwenye jengo. Mungu awabariki. Hilo ni jema. Loo, ni vibaya sana hatuna mwezi mmoja kuwa hapa. Mnaona, acheni tu . . . Mimi ni mgeni kwenu. Mnaona, ni vigumu. Ninyi endeleeni tu kuamini.

201 Sasa, ni Nuru. Mungu ni Nuru, tunajua hilo, Nguzo ya Moto. Basi sasa wewe omba tu ukaiguse Hiyo, na ninaomba Bwana Yesu ajibu.

202 Sasa ninachukua kila roho hapa ndani chini ya mamlaka yangu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya utukufu Wake. Sasa iweni na kicho kabisa. Ombeni. Iweni na kicho kabisa.

203 Sasa, Hii hapa. Yupo mama papa hapa mbele yangu. Ameinamisha kichwa chake, naye anaomba kwa ajili ya mateso yake mwenyewe. Kama unataka kuinua kichwa chako sasa, yupo papa hapa mbele yangu. Je! unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini kwamba Mungu anaweza kukiponya hicho kisukari na kukupa afya? Sasa, hicho ndicho ulicho nacho, kisukari. Sikujui mimi. Wewe ni mgeni kabisa kwangu mimi. Lakini je! unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Iwapo—iwapo hatufahamiani mmoja na mwingine, inua mkono wako, namna *hiyo*, kusudi watu waone. Mnaona? Vema. Mnaona, huyu hapa mama huyo. Na sasa anaugua ugonjwa wa kisukari. Na unaamini kwamba Mungu anaweza kuniambia kuwa wewe ni nani? Ingekufanya uamini? Wewe ni Bibi Martin. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaona? Wewe kuwa tu na imani. Usitie shaka. Kuwa na imani.

204 Sasa yeye aligusa nini? Ninataka kuwauliza wasikilizaji. Aligusa nini? Hapo yupo mwanamke ameinua mkono wake wa kuume, na wangu, pia, mbele za Mungu. Mnaona? Aligusa Kitu fulani. Maskini mwanamke wa kawaida tu, hiyo hakika, kuwaambia kweli, sasa mwone kama hii ni kweli, ilimshangaza. Hakujua alikuwa na imani kiasi hicho. Imani si kitu unachojiundia; ni kitu ulicho nacho. Mnaona? Alishangazwa. Hata sasa hivi mwanamke huyo anajihisi tofauti na alivyohisi dakika chache zilizopita. Anajua jambo fulani limetendeka kwake.

205 Hapa, hivi hamwioni hiyo Nuru? Sawa. Mnaiona papa hapa juu ya mwanamke huyu hapa, papa hapa nyuma? Anaugua . . . Amekiinamisha kichwa chake. Anaomba. Lakini anateseka na tatizo la mgongo wake. Ikiwa ataamini kwa moyo wake wote, anaweza kuponywa tatizo hilo la mgongo. Hakika.

206 Atalikosa, kwa hakika kabisa kama chochote. Unaona, maombi yake yangali yanasonga. Bwana, nisaidie. Bibi DeVille, ni wewe. Hiyo ni neema. Mwanamke huyo alikuwa anaomba, hata hakuwa akiwazia, hata hanisikii nikisema chochote. Sasa wewe mwulize kama ananijua. Hilo ndilo jina lake, na hilo ndilo tatizo lake.

207 Basi aligusa nini? Hilo ni thibitisho la Yesu Kristo, Neno, hutambua mawazo yaliyoko moyoni.

208 Je! Mnaamini? Iweni tu na imani. Ombeni, popote pale. Aminini tu. Hayo ndiyo yote yakupasayo kufanya. Aminini tu, aminini tu kwamba nimewaambia Kweli. Sasa, mimi si Yeye. Mimi tu ni mtumishi Wake, mtumishi Wake tu.

209 Laiti mngalikuwa na imani ya kutosha! Siwezi kumwita. Ninajua shida yake, ila, unaona, ngojea tu kidogo na labda itabadilika. Kwa kweli si jambo lisilowezekana, bali inakubidi kuondoka kwenye kiwango hicho. Yeye hawezi kuamini kwa ajili yake mwenyewe. Huna budi kuamini kwa ajili yake.

210 Mwanamke anayeugua tatizo la figo. Hatoki hapa. Anatoka Mississippi. Ataamini kwa moyo wake wote, Mungu ataliponya hilo tatizo la figo. Bibi Palmer, kama utaamini kwa moyo wako wote, unaweza kuponywa hilo. Limekuacha. Aligeuza Nuru juu yake. Limemwacha. Mwamini Mungu. Usitie shaka.

211 Yupo mama anayeketi karibu naye. Anasumbuliwa na ugonjwa wa baridi yabisi. Je! unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu, mama? Unaamini? Je! unaamini kama Mungu ataniambia wewe ni nani, je! hiyo itakusaidia kuamini? Jina lako ni Bibi Meadow. Wewe amini kwa moyo wako wote sasa, unaweza kuponywa, pia.

212 Hiyo ilishika moto kwa mama anayeketi karibu na yeye. Ameketi hapo, pia. Hiyo hapo inaenda, moja kwa moja kwenye mstari. Mama aliyeketi pale, yeye anaugua. . . Karibu naye, anaugua kisukari, ugonjwa wa kisukari. Wanamtaka aende kwenye hospitali, lakini anakataa kuenda. Anaye mwana anayemwombea, pia. Huyo mwana hayupo hapa, lakini je! unaamini Mungu anaweza kuniambia shida ya huyo mtoto? Ana tatizo la moyo. Wewe amini, Naye atakuponya. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Bibi Dufflee, D-u, f maradufu, l, e maradufu. Namna fulani . . . Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, huku umeinua mikono yako. Vema. Sasa wewe amini, nawe unaweza kuponywa, pia.

213 Je! unaamini kwamba hicho ndicho kitu kile kile ambacho ninii . . . Mnaamini kwamba Uwepo wa Yesu Kristo upo hapa sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ni wangapi wanaokubali hilo? ["Amina."] Loo, ni usalama jinsi gani! Ni usalama jinsi gani! Mnaona?

214 Mlifanya nini? Mlimwamsha. Mlimleta jukwaani. Huyu hapa jukwaani. Hiyo haileti tofauti yoyote kile mashua zinasema. Kumbukeni, Yeye anaweza kusema, "Amani, tulia."

215 Je! mnaamini hilo kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linashangilia na kusema, "Amina."—Mh.] Kama mnaamini, simameni kwa miguu yenu na mlikubali. Simama na useme, "Ninaamini hilo kwa moyo wangu wote." Simama moja kwa

moja kwa miguu yako. "Ninaamini sasa." Hiyo ni kweli, haijalishi ni nini tatizo lako, simama, mpe Sifa.

216 Baba wa Mbinguni, tunakuletea Wewe kusanyiko hili. Wanatambua ya kwamba Wewe upo hapa, Bwana.

Naomba kila pepo, kutokuamini, aondoke mahali aliposhikilia, na hebu Yesu Kristo awaponye nyote.

217 Shetani, toka ndani ya wasikilizaji hawa! Katika Jina la Yesu Kristo, umekataliwa.

KUMWITA YESU JUKWAANI SWA64-0319
(Calling Jesus On The Scene)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, tarehe 19 Machi, 1964, katika Shule ya Sekondari ya Denham Springs kule Denham Springs, Louisiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org